

# **Azimio la Uwajibikaji wa Kitaaluma Mkataba wa Kijamii na Kibinadamu katika Utabibu**

## **Dibaji**

Hakuna wakati mwingine katika historia ya maendeleo ya kibinadamu ambapo maslahi ya kila mtu yanahusishwa na ya wenzake. Mapigo na majanga hayaheshimu mipaka ya kimataifa katika ulimwengu wa utandawazi wa kibiashara na safari. Vita na matendo ya kigaindi yanawafanya watu wasio na hatia kuwa wapiganaji na raia kuwa shabaha. Ingawa Maendeleo katika sayansi ya kimatibabu na jeni yanaahidi matokeo mazuri, yanaweza kutumiwa visivyo na kama maajenti wa maovu. Kutokana na uwezo usiokadirika pamoja na dharura inayosababishwa na changamoto hizi, pana haja ya kila mtu kuchukua hatua zifaazo.

Kama matabibu, tunajukumika katika kazi yetu kutokana na desturi ya kuwahudumia wagonjwa na wale wanaotaabika. Kwa karne nyingi, matabibu binafsi wametokeleza wajibu huu kwa kutumia ujuzi na maarifa yao vizuri, bila ubinafsi na wakati mwingine kishujaa. Kwa sasa, taaluma yetu ni lazima idhibitishe kujitolea kwake kunakofahamika ili kukabiliana na matatizo ya kimaumbile na ya kibinadamu pamoja na maslahi ya kibinadamu. Ni katika kutenda pamoja kwa kukiuka mipaka ya kijiografia na kimawazo ndio tutaweza kuhimili vikwazo vikubwa. Ubinadamu ndio mgonjwa wetu.

## **Azimio**

Sisi, wanachama wa jamii ya ulimwengu ya matabibu, tunajitolea kwa dhati:

1. Kuheshimu maisha ya binadamu pamoja na hadhi ya kila mtu
2. Kujizuia kuunga mkono au kutekeleza uhalifu dhidi ya binadamu na kukemea matendo kama hayo.
3. Kuwatibu wagonjwa na waliojeruhiwa kwa upendo na bila uonevu.
4. Kutumia maarifa yetu na ujuzi wakati inapohitajika hata kama kufanya hivyo kutahatarisha maisha yetu.
5. Kulinda usiri na faragha kwa wale ambao tunawahudumia na kukiuka usiri huu pale tu ambapo kuhifadhi siri kutakuwa kunahatarisha afya na usalama wao au wa wengine kwa njia kubwa.
6. Kufanya kazi kwa uwazi na wafanyakazi-wenza ili kutambua, kuendeleza na kuimarisha maendeleo katika utabibu na afya ya umma yanayoondoa mahangaiko na kuimarisha afya ya binadamu.
7. Kuelimisha umma na serikali kuhusiana na hatari za sasa na za baadaye kwa afya ya binadamu.
8. Kutetea mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, kielimu na kisiasa yatakayoondoa mahangaiko na kuimarisha hali nzuri ya kibinadamu.
9. Kuwafunza na kuwaelekeza wale wanaotufuata kwani wao ndio mustakabali wa taaluma yetu ya kuwahudumia wengine.

Tunatoa ahadi hizi kwa dhati, bila malipo, na kwa heshima yetu binafsi na ya taaluma yetu